JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU
SERA, URATIBU, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# MKATABA WA UNUNUZI WA KANDARASI ZA UJENZI

KATI YA

KATIBU MKUU, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

NA

TAASISI YA TEKNOLOJIA YA DAR ES SALAAM - ICB

Namba ya ZABUNI: ME 003/2021-22/W/8

UKARABATI NA UPANUZI WA CHUO CHA WATU WENYE ULEMAVU - YOMBO

January 2022

I) FOMU YA MKATABA

# FOMU YA MAKUBALIANO YA ZABUNI

Makubaliano haya ya zabuni ya nafanywa leo siku ya ...18......, Mwezi wa......01.........Mwaka wa.......2022...... Kati ya **Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, S. L. P. 2890** Dodoma (Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja na **Taasisi ya Teknolojia ya Dar Es Salaam - ICB wa S.L.P. 2958 Dar Es Salaam** (Hapa ataitwa "Fundi") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Fundi anakaribisha zabuni kwa kutoa huduma yaani: ukarabati wa majengo ya chou cha Watu wenye Ulemavu Yombo na amekubali Kazi ya Ukarabati kupitia Zabuni Na. ME 003/2021-22/W/8 kwa jumla ya **Shilingi za Tanzania Milioni Mia Moja Arobaini na Mbili, Mia Nne Hamsini Elfu, Mia SabaThemanini na Nne tu (TZS 142,450,784/=)** Hapa itaitwa ("Bei ya Mkataba").

SASA MAKUBALIANO HAYA YAMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:

1. Katika makubaliano haya maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaojieleza.

2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya makubaliano haya, yaani;
   - i) Fomu ya Mkataba
   - ii) Fomu ya Kuwasilisha zabuni;
   - iii) Barua ya wito wa kukubaliwa zabuni.
   - iv) Uainishaji Viwango na Vipimo Kiufundi, kama upo;
   - vi) Maelezo ya Mahitaji na Orodha ya gharama;
   - vii) Michoro
   - vii) Mhutasari wa majadiliano.

3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejewa kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilisha na zinajieleza zenyewe lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyooneshwa hapo juu.

4. Katika kuzingatia malipo yatakayofanywa na **Mwajiri** kwa **Fundi** kama baadaye inavyotajwa, **Mwajiri** hapa anakubaliana na **Fundi** kutekeleza na kukamilisha huduma na kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza kwa kuzingatia masharti ya Mkataba huu.

5. Kwamba, **Fundi** atawajibika kumlipa **Mwajiri** hasara za vifaa vyote pamoja na gharama nyinginezo zitakazotokana na kazi zisizoridhisha kwa mujibu wa Mkataba huu.

6. Kwamba, **Fundi** atalipa **Mwajiri** asilimia thelathini (30%) ya kazi ambayo hajamaliza kwa wakati itakayosababisha Mwajiri kuingia gharama nyingine ya ziada.

7. Kwamba, vifaa vyote vya ujenzi (Building materials) vitatolewa na **Mwajiri** na **Fundi** atalipwa gharama za ufundi tu (Labour charge). Vifaa vya kufanyia kazi (kama mwiko, pima maji, kamba, tape measure nk. ni vya Fundi mwenyewe).

8. Kwamba, **Fundi** awe na fedha ya kuanzia ya kulipa vibarua na awe na akaunti ya



KD  JK

benki.

9. Kwamba, kwa kuzingatia malipo yatakayofanywa na **Mwajiri** kwa **Fundi** kama ilivyotajwa katika Mkataba huu, **Mwajiri** anakubaliana na **Fundi** kutekeleza na kukamilisha kazi ya ujenzi na kurekebisha kasoro zozote zitakazojitokeza kwa kuzingatia masharti ya Mkataba huu.

10. Kwamba, **Mwajiri** anakubali kumlipa kiasi cha **Shilingi za Tanzania Milioni Mia Moja Arobaini na Mbili, Mia Nne Hamsini Elfu, Mia SabaThemanini na Nne tu (TZS 142,450,784/=** bila Kodi ya Ongezeko la Thamanai kwa kazi ya ukarabati wa majengo ya Chuo cha Watu wenye Ulemavu - Yombo kwa muda wa **Miezi Sita (6).**

11. Kwamba, malipo yatafanyika kwa kila hatua ya ujenzi iliyokamilika na kukaguliwa. Malipo ya hatua ya ujenzi iliyokaguliwa na kuthibitishwa na Mhandisi wa ujenzi yatafanyika na Mwajiri ndani ya siku thelathini (30) tangu siku ya kuthibitishwa kwa kazi inayoombewa malipo.

12. Kwamba, Mkataba huu utakuwa wa Miezi 6 na **Fundi** ataanza kazi tarehe

.................. na kumaliza tarehe .......................

**KWA USHUHUDA**, pande hizi zimefanya makubaliano ya kutekeleza Mkataba huu kwa siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

| **KWA NIABA YA MWAJIRI:** | **MBELE YA:** |
|---|---|
| ............................ **Saini** | ............................ **Saini** |
| (Jina) JAMAL A. KATUNDU | (Jina) JANUARY KITUNSI |
| (Kazi) KATIBU MKUU | (Kazi) AFISA SHERIA |
| (Muhuri wa Ofisi): .................... | |

| **KWA NIABA YA FUNDI:** | **MBELE YA** |
|---|---|
| ............................ **Saini** | ............................ **Saini** |
| (Jina) ANDERSON A. TOUO | (Jina) NELSON MDELWA |
| (Kazi) ARCHITECT | (Kazi) AFISA SHERIA |
| (Anwani) 275 SOUTH... | (Anwani) 2958 DSM |
| (Muhuri wa Ofisi) .................. | |

ARCHITECTS AND QUANTITY SURVEYORS REGISTRATION BOARD TANZANIA
APL 264.324.9/19
Sign:

## (ii) MASHARTI MAALUM YA MKATABA WA UNUNUZI

## MASHARTI MAALUM YA MKATABA (MMM)

Masharti haya Maalum ya Mkataba ni nyongeza ya Masharti ya Jumla ya Mkataba. Pale patakapotokea mgogoro, masharti haya yatakuwa na nguvu juu ya Masharti ya Jumla ya Mkataba. Isipokuwa pale itakavyobainishwa vinginevyo, Masharti yote Maalum ya Mkataba yatajazwa na Mwajiri kabla ya kutolewa kwa Nyaraka za Zabuni. Jedwali na taarifa zitakazotolewa na Mwajiri zitaambatishwa.

| Kifungu cha Masharti Maalum ya Mkataba. | Kifungu cha Masharti ya Jumla ya Mkataba | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | 1.1 & 7.0 | **A. Maelezo ya Jumla**<br>Mwajiri ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, S. L. P. 2890, Dodoma.<br><br>Mamlaka iliyoteuliwa na Msuluhishaji: **Tanzania Institute of Arbitrators.**<br><br>Kipindi cha Marekebisho ya Dosari ni siku ***180***<br>Meneja Mradi ni; Bw. Wenceslaus Lambileki:<br><br>Jina na Namba ya Utambulisho wa Mkataba ni;<br>**Namba ya ZABUNI: ME 003/2021-22/W/8.**<br>**Ukarabati na Upanuzi wa Chuo cha Watu Wenye Ulemavu – Yombo.**<br>Kandarasi inajumuisha; ***Kufanya kazi za ukarabati wa majengo ya Chuo* cha Watu Wenye Ulemavu - Yombo *kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba.***<br>Tarehe ya Kuanza Kazi ____________________.<br>Muda uliokusudiwa kumaliza kazi ni ***Miezi 6 (sita).***<br>Eneo la Kazi lipo ***Yombo – Dar Es Salaam*** na imetafsiriwa katika michoro Na. ____________________ |



XA J.K

| Kifungu cha Masharti Maalum ya Mkataba. | Kifungu cha Masharti ya Jumla ya Mkataba | Maelezo |
| --- | --- | --- |
| 2. | 2.2 (k) | Nyaraka nyingine zinazounda sehemu ya Mkataba, kama zipo [*orodhesha nyaraka*]: |
| 3. | 15.1 | Kima cha chini cha bima kinahusisha:<br>(a) Upotevu wa, au uharibifu wa Kandarasi, Karakana, na Vifaa **TZS 5,000,000/=**<br>(b) Upotevu wa, au uharibifu wa Mitambo<br>**TZS *5,000,000/=***<br>(c) Upotevu wa, au uharibifu wa (isipokuwa kandarasi, Karakana, Material, na Mitambo) **TZS *5,000,000/=,***<br>(d) Ajali au kifo ***1,000,000/=*** |
| 4. | 22 | Utekelezaji wa kandarasi utaanza na kumalizika katika kipindi cha *miezi* ***Sita (6)*** |
| 5. | 25.1 | Kiasi cha malipo ya awali ni asilimia ***20*** ya gharama za mkataba zitakazolipwa ndani ya ***siku 14*** baada ya kuwasilisha dhamana ya mkopo inayokubalika kibenki au Bima [Bank Guarantee or Insuarance Bond]. |
| 6. | 25.2 | Kiasi cha chini cha malipo ya awamu kitakuwa ***50,000,000/=*** |
| 7. | 25.2 | Kiasi cha fedha kitakachozuiliwa ni ***10%*** ya thamani ya kandarasi zenye malipo ya awamu. |
| | | Kikomo cha fedha zilizozuiliwa kitakuwa asilimia ***80*** ya bei ya mkataba. |
| 8. | 25.3 | Kiwango cha Riba kitakuwa asilimia ***Haitumiki*** **(N/A)** ya tarehe benki ya biashara ya mkandarasi. |
| 9. | 25.4 | Kiwango cha riba kwa malipo yatakayochelewa ni ***Haitumiki*** **(N/A)** |
| 10. | 27.1 | Msuluhishaji aliyeteuliwa ni ***Atateuliwa na Mamlaka ya Uteuzi Iliyopendekezwa*** |
| 11. | 27.2 | Muda wa usuluhishi ni ***Siku 28*** |



AA J.K

| Kifungu cha Masharti Maalum ya Mkataba. | Kifungu cha Masharti ya Jumla ya Mkataba | Maelezo |
|---|---|---|
| 12. | 27.3 | Muamuzi aliyeteuliwa; ***Atateuliwa na Mamlaka ya Uteuzi iliyopendekezwa*** |
| 13. | 27.4 | Taasisi ya Uamuzi ni **Tanzania Institute of Arbitrators**<br><br>Mahali pa kufanyia Uamuzi ni **Dodoma** |

## (iii) MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA (MJM)

| A: VIFUNGU | |
|---|---|
| 1. | **Tafsiri ya Maneno** |
| | Maelezo yafuatayo katika Masharti ya Jumla ya Mkataba yanatoa maana kama ifuatavyo:<br><br>**Hati ya Kukamilisha Marekebisho:** ni hati inayotolewa na Meneja wa Mradi baada ya Mkandarasi kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa kwenye mradi.<br><br>**Kasoro:** ni sehemu ya kazi yoyote ambayo haijaisha kulingana na matakwa ya Mkataba.<br><br>**Kazi:** inamaanisha kazi zitakazofanywa kulingana na matakwa ya mkataba.<br><br>**Makadirio ya Kazi** ni mchanganuo na makisio ya bei ya makadirio ya Kazi ambayo ni sehemu ya Zabuni.<br><br>**Meneja wa Mradi** ni mtu anayetajwa katika MMM (au mtu yeyote mahiri aliyeteuliwa na Mwajiri na uteuzi wake kutaarifiwa kwa Mkandarasi, kufanya kazi kwa niaba ya Meneja wa Mradi) ambaye anawajibika kusimamia utekelezaji wa kazi pamoja na usimamizi wa Mkataba.<br><br>**Mkandarasi Msaidizi** ni mtu binafsi au kampuni anayeweza kushitaki au kushitakiwa kisheria na ambaye ana Mkataba na Mkandarasi au Mwajiri kufanya baadhi ya kazi zilizopo kwenye Mkataba, ambazo zinajumuisha kazi zilizopo kwenye eneo la kazi.<br><br>**Mkandarasi** ni mtu binafsi anayeweza kushitaki au kushitakiwa kisheria ambaye zabuni yake imekubaliwa na mwajiri.<br><br>**Mkataba** ni makubaliano kati ya Mwajiri na Mkandarasi kufanya kazi zilizoainishwa, kumaliza kazi na kufanya matengenezo ya kazi husika. |



J-K

| | |
|---|---|
| | Mkataba unajumuisha makabrasha yaliyoorodheshwa katika **MJM 2.2.**<br><br>**Msuluhishi** ni mtu atakayeteuliwa na mamlaka teuzi kama inavyoainishwa katika Masharti Maalum ya Mkataba (**MMM**) ili kusuluhisha migogoro ya kimkataba na kama inavyoainishwa kwenye **MJM 25.1.**<br><br>**Muda wa Matazamio wa Marekebisho:** ni muda uliotajwa kwenye **MMM** na unahesabiwa kuanzia tarehe ya kumaliza mradi.<br><br>**Mwajiri** ni Taasisi ya Serikali inayonunua huduma kama ilivyoainishwa katika Maalum ya Mkataba (**MMM)**<br><br>**Tarehe Iliyokusudiwa ya Kumaliza Kazi: ni** tarehe inayokusudiwa kuwa Mkandarasi atakuwa amemaliza kazi. **Tarehe Iliyokusudiwa ya Kumaliza Kazi** imeaninishwa kwenye **MMM**.<br><br>**Tarehe Rasmi ya Kuanza Mkataba:** ni tarehe inayoonyeshwa kwenye Tuzo ya Kuanza kwa utekelezaji wa Mkataba inayotolewa na Mwajiri baada ya kuzingatiwa kwa masharti tangulizi kama inavyobainishwa kwenye **MJM 3.**<br><br>**Tarehe ya Kuanza Kazi** ni tarehe ambayo Mkandarasi atakayoanza kufanya kazi kama inavyoainishwa kwenye Tuzo ya Mkataba wa Kuanza Kazi. Tarehe ya kuanza Kazi inaweza kurekebishwa na Meneja wa Mradi kwa kushauriana na mwajiri kwa kutoa notisi ya kuongeza muda.<br><br>**Tarehe ya Kumaliza Kazi** ni tarehe ya kumaliza kazi kama ilivyopitishwa na Meneja wa Mradi kulingana na MJM 20. |
| **2.** | **Tafsiri ya Masharti na Nyaraka za Mkataba** |
| | 2.1 Katika kutafsiri Masharti haya ya Mkataba, Vichwa vya habari na maelezo ya pembeni yatatumika kwa kadiri inavyofaa na hayatoathiri tafsiri zake isipokuwa pale itakapobainishwa: marejeo ya umoja itamaanisha pia wingi au kinyume chake; na jinsi ya kiume inajumuisha pia jinsi ya kike au kinyume chake. Maneno yaliyotumika katika Mkataba huu yatabeba maana zake za kawaida katika lugha za Mkataba isipokuwa pale yanapotafsiriwa vinginevyo.<br><br>2.2 Nyaraka mbalimbali zinazounda Mkataba; kila waraka utachukuliwa |

| | |
|---|---|
| | kama unaelezea mwingine. Lakini panapotokea ukinzani, kipaumbele cha nyaraka kitazingatia mpangilio wa nyaraka hizo kama ifuatavyo:<br>(a) Fomu ya Makubaliano ya ununuzi;<br>(b) Barua ya Kukubali;<br>(c) Muhtasari wa Kikao cha Majadiliano (kama yalikuwepo);<br>(d) Fomu ya Kuwasilisha Kotesheni;<br>(e) Masharti Maalumu ya Mkataba;<br>(f) Masharti ya Jumla ya Mkataba;<br>(g) Tuzo ya Kuanza kwa Mkataba;<br>(h) Viwango na Vipimo;<br>(i) Michoro;<br>(j) Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi; na<br>(k) Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba kama zilivyoorodheshwa kwenye **MMM**. |
| **3.** | **Maelekezo** |
| | Maelekezo yanayotolewa na Mwajiri kwa Mkandarasi kupitia Meneja Mradi yatatolewa kwa njia ya maandishi au kwa njia ya kielektroniki na endapo kwa sababu yoyote maelekezo hayo yatatolewa kwa njia ya mdomo, Mtoa Huduma atazingatia maelekezo hayo. Ndani ya kipindi cha siku saba (7), maelekezo hayo ya mdomo yatathibitishwa kwa maandishi au kwa njia ya kielektroniki inayotunza kumbukumbu. |
| **4.** | **Lugha** |
| | Notisi zote, maelekezo, mawasiliano au nyaraka zozote za kimaandishi zinazohusiana na Mkataba zitakuwa katika lugha ya Kiswahili. |
| **5.** | **Sheria inayotumika** |
| | Mkataba, maana yake, tafsiri yake na utekelezaji wake vitaongozwa na Sheria za Tanzania. |

| | |
|---|---|
| **6.** | **Majukumu ya Mhandisi /Meneja wa Mradi** |
| | Bila kuathiri masharti mengine yoyote, Meneja wa Mradi atasimamia utekelezaji wa mkataba kati ya Mwajiri na Mkandarasi. Meneja wa Mradi hana mamlaka kisheria kurekebisha mkataba. |
| **7.** | **Mawasiliano** |
| | Mawasiliano baina ya pande zinazohusika za Mkataba yatakuwa yamekamilika iwapo tu yatakuwa kwa njia ya maandishi au kielektroniki inayotunza kumbukumbu ya yaliyomo ndani ya mawasiliano hayo. Notisi itakuwa imekamilika iwapo tu imewasilishwa kwenye anuani iliyoainishwa kwenye **MMM.** |
| **8.** | **Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba** |
| | 8.1 Mkandarasi atatakiwa kuwasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba (lililoambatanishwa **Sehemu ya Saba)** ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kukamilika kwa masharti ya kabla ya kusaini mkataba, baada ya kupokea barua ya tuzo na kabla kusainiwa Mkataba.<br><br>8.2 Endapo Mkandarasi atashindwa kutekeleza majukumu ya Mkataba Mwajiri atawasilisha mapendekezo ya kumfungia Mkandarasi huyo kulingana na matakwa ya Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba.<br><br>8.3 Uhalali wa Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba utafikia ukomo wake baada ya siku thelathini (30) baada ya Mkandarasi kukamilisha utekelezaji wa majukumu yake chini ya Mkataba. |
| **B:** | **MAJUKUMU YA JUMLA YA MKATABA** |
| **9.** | **Utekelezaji wa Kazi** |
| | Mkandarasi atatoa nguvu kazi yote, zana , mitambo, usafiri, vifaa na cho chote kile kinachohitajika kwa ukamilishaji wa kazi ikiwa ni pamoja na maji na umeme. Atafanya kazi kulingana na masharti ya nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakavyotolewa mara kwa mara. |
| **10.** | **Hali Mbaya ya Ukinzani** |



AA J-K

| | |
|---|---|
| | Endapo wakati wa utekelezaji wa kazi Mkandarasi atakabiliana na hali mbaya ya ukinzani ambayo haihusiani na hali ya hewa na ambayo haikuweza kutarajiwa na Mkandarasi, Mhandisi ataamua nyongeza ya muda unaostahili ambao Mkandarasi atastahili kupewa. |
| **11.** | **Kutoa kazi kwa Mkandarasi Msaidizi** |
| | Kwa idhini ya Mwajiri, Meneja Mradi anaweza kumruhusu Mkandarasi kutoa sehemu ya kazi ya kimkataba kwa Mkandarasi Msaidizi. Kutoa sehemu ya kazi kwa Mkandarasi msaidizi hakutabatilisha majukumu ya jumla ya Mkandarasi. |
| **12.** | **Usimamizi wa Kazi Unaofanywa na Mkandarasi** |
| | Mkandarasi atatekeleza kazi kwa uangalifu na weledi na kwa kufuata viwango vilivyowekwa na Mhandisi/Meneja Mradi ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, wingi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mhandisi akibaini uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo kutoka mienendo iliyowekwa, hatua zinazofaa zitachukuliwa na Mkandarasi ili kurekebisha hali hiyo. |
| **13.** | **Ukaguzi** |
| | Mhandisi au mwakilishi wake aliyempa mamlaka anayo haki ya kukagua kazi ili kuangalia kama inakidhi viwango vilivyowekwa na Mwajiri na Mkandarasi atatoa usaidizi unaofaa kwa shughuli hiyo na kwa wakati Mhandisi atakapohitaji. |
| **14.** | **Kazi Zinazokataliwa**<br>Kazi ambazo hazikuzingatia vigezo vilivyowekwa pamoja na masharti ya mkataba zitakataliwa. Kwa kufuata maelekezo ya Meneja Mradi, Mkandarasi atatengeneza au kurekebisha au kufanya upya kazi itakayokuwa imekataliwa hadi itakapomridhisha Mhandisi kikamilifu kwa gharama zake mwenyewe |
| **15.** | **Bima** |
| | 15.1 Mkandarasi atatakiwa kutoa bima kwa majina ya pamoja ya Mwajiri na |

| | |
|---|---|
| | Mkandarasi, dhamana ya bima, kuanzia tarehe ya mwanzo na mwisho ya Muda wa Maangalizi baada ya mradi kumalizika kwa kiasi na makato yaliyobainishwa katika **MMM** kwa matukio ya tahadhari ambayo yatakuwa upande wa Mkandarasi, hasara au uharibifu kwenye vifaa na mitambo ya Mkandarasi na ulipaji wa fidia ya majeruhi na vifo.<br><br>15.2 Mkandarasi atatakiwa kupeleka Sera na tuzo za bima kwa Meneja Mradi ili aidhinishe kabla ya kuanza kutumika. Bima hizi zinatakiwa kuonesha aina, kiasi na sarafu ya ulipaji wa mafao kwa kufidia hasara au uharibifu utaofanyika.<br><br>15.3 Iwapo Mkandarasi hatoi aina yoyote ya sera na tuzo za bima zinazohitajika, Mwajiri anaweza kulipa bima hizo ambazo Mkandarasi angetakiwa kuzilipa na na atakata gharama alizoingia kupitia kwa malipo ya Mkandarasi kama yapo au litakuwa ni deni la Mkandarasi.<br><br>15.4 Marekebisho kwenye matakwa ya bima hayatoweza kufanyika bila ya indini ya Mwajiri kupitia kwa Meneja wa Mradi.<br>15.5 Pande zote zitatakiwa kukidhi masharti yoyote ya Sera za Bima |
| **16.** | **Madeni ya Mkandarasi** |
| | Mkandarasi hatamhusisha Mwajiri dhidi ya madai yoyote yanayotokana na hasara au uharibifu wa upande wa tatu (third party). Atamkinga kikamilifu Mwajiri wake dhidi ya madeni (liabilities) yanayotokana na Sheria za Ajira. |
| **17.** | **Tukio Lisilotarajiwa** |
| | 17.1 Bila kuathiri matakwa ya vifungu vya MJM 24 na 26, Mkandarasi hatawajibika kukatwa asilimia ya fedha kwa kutowajibika kimkataba, au kufukuzwa kazi kwa makosa yaliyojitokeza kuchelewesha utekelezaji wa mradi au kushindwa kutekeleza majukumu yake kimkataba kutokana na tukio lisilotarajiwa;<br><br>17.2 Kwa ajili ya matakwa ya kifungu hiki cha MJM "Tukio lisilotarajiwa" ni tukio lililo nje ya uwezo wa Mkandarasi na halihusishi makosa ya Mkandarasi au uzembe na halitabiriki. Matukio kama haya yanajumuisha |

| | |
|---|---|
| | pamoja na vitendo vya Mwajiri vya kuhatarisha amani ya nchi, vita au mapinduzi, moto, mafuriko, milipuko ya magonjwa, karantini maalum na zuio la kimataifa la mizigo;<br><br>17.3 Kama hali ya tukio lisilotarajiwa likitokea, Mkandarasi atatakiwa mara moja kumtaarifu Mwajiri kwa maandishi. Kama Mwajiri hatajibu vinginevyo kuhusu taarifa hiyo, Mkandarasi atatakiwa kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kimkataba kama atakavyoona inafaa na atatafuta njia nyingine mbadala za utelekelezaji wa mradi ambazo haitaathiriwa na tukio lisilotarajiwa;<br><br>17.4 Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa aina yoyote wa nguvu za asili ambao pande za mkataba hazikuweza kufikiria mapema, Mkandarasi atarekebisha hasara au uharibifu. Mwajiri ataaamua kutoa ziada ya Bei ya Mkataba na pia anaweza kufikiria kutoa muda wa nyongeza wa kipindi cha mkataba. |
| **18.** | **Ubora wa Vifaa na Utendaji Kazi** |
| | Vifaa vyote na usanifu wa kazi vitakuwa vya aina na ubora kama ilivyofafanuliwa katika mkataba na pia kulingana na maelekezo ya Mhandisi na vitapimwa kama Mhandisi atakavyoona inafaa. Mkandarasi atatoa bure msaada unaohitajika kwa ajili ya kupima ubora wa vifaa na atakuwa na wajibu wa kugharimia upimaji wote utakaohitajika. |
| **19.** | **Upatikanaji wa Vifaa** |
| | Mkandarasi atabainisha vyanzo vyote vya vifaa yanavyohitajika kabla ya kuanza kwa kazi. Pale itakapohitajika, Mwajiri atawezesha upatikanaji wa vyanzo hivyo. Mkandarasi hatatakiwa kutumia vifaa bila kupata kwanza idhini ya maandishi kutoka kwa Mhandisi. |
| **20.** | **Usafishaji wa Eneo la Kazi** |
| | Baada ya kumaliza kazi, Mkandarasi ataondoka kutoka eneo la kazi mitambo yote, vifaa vyote, zana zote, na vifaa vilivyosalia , takataka na kazi za muda na ataacha eneo la kazi likiwa safi na katika hali inayoridhisha. |



XA J-K

| | |
|---|---|
| **21.** | **Afya, Usalama na Kulinda Mazingira** |
| | Katika kipindi chote cha mkataba, Mkandarasi atatakiwa kuzingatia hali ya afya, na usalama katika eneo lake la kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari kwa watu hao. Mkandarasi atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira zilizopo kama zinavyoelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |
| **22.** | **Kuanza na Kukamilika kwa Kazi**. |
| | Mkandarasi ataanza na kukamilisha kazi katika muda uliyoelezwa kwenye **MMM** au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mwajiri. |
| **23.** | **Mabadiliko ya Mawanda ya kazi** |
| | Kwa idhini ya Mwajiri, Mhandisi anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha kazi na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Mkandarasi ipasavyo. Mabadiliko hayo yatafanywa kwa Agizo la Mabadiliko katika Mkataba. Mhandisi ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na kiwango cha kizio au kama hakuna kiwango cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mhandisi na kukubaliwa na wote, Mwajiri na Mkandarasi. |
| **C:** | **MALIPO** |
| **24.** | **Kiasi** |
| | Kiasi kilichowekwa kwenye mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ni kiasi kilichokadiriwa kwa kazi na kisichukuliwe kuwa ndiyo kiasi halisi sahihi kitakachotumiwa na Mkandarasi.<br><br>Mhandisi ataamua kwa kupima thamani ya kazi halisi na taidhinisha malipo ya kazi yanayoendana na kazi iliyofanyika na kupimwa kwa kwa kiasi cha |



AB J-K

| | |
|---|---|
| | gharama iliyowekwa kimkataba.<br><br>Mabadiliko ya mkataba kwa kiasi kilichoongezeka kwa kipengele kinachofanana na yatatumia bei ile ile kama inavyoonyesha kwenye mkataba wa awali.<br><br>Iwapo kiasi cha mwisho cha kazi iliyofanyika kinatofautiana na kiasi kilichopo kwenye makadirio ya gharama kwa kipengele husika kwa zaidi ya asilimia 25 kama ongezeko hilo linazidi asilimia 1 ya bei ya mkataba wa mwanzo, Mhandisi au Meneja wa Mradi atarekebisha kiwango ili kuruhusu mabadiliko hayo kwa kumshirikisha Mwajiri na kupata idhini yake.<br><br>Endapo mwajiri ataridhia, Mhandisi au Meneja wa Mradi atabadilisha viwango kutokana na mabadiliko ya kiasi na kama bei ya awali ya mkataba haijazidi kwa asilimia 15. Iwapo badiliko limezidi kwa asilimia 15, idhini inabidi iombwe kutoka kwenye mamlaka inayoidhinisha bajiti ya mwajiri. |
| **25.** | **Malipo** |
| | 25.1 **Malipo ya Awali**<br><br>Malipo ya Awali ya **asilimia 20** ya thamani ya mkataba **yanaweza** kutolewa kama itakuwa inaonyesha hivyo kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba** baada ya kuwasilisha dhamana ya mkopo inayokubalika. Malipo ya awali yatakatwa pole pole kwa mafungu sawa kwa kila madai yatakayowasilishwa na Mkandarasi kwa malipo, mpaka malipo ya awali yote yatakaporudishwa kikamilifu.<br><br>25.2 **Malipo ya Kati**<br><br>Malipo yatafanywa na Mkandarasi kwa cheti cha malipo ya kati kama kazi iliyokamilika imefikia viwango vilivyowekwa kwenye Mkataba. Kwa cheti cha malipo ya kati, kiasi cha fedha kilichotajwa kwenye **MMM** kitashikiliwa kwa kiasi kisichozidi asilimia kumi (10%) ya bei ya mkataba. Asilimia hamsini (50%) ya Fedha hiyo iliyoshikiliwa italipwa katika cheti cha malipo ya mwisho. Na asimilia iliyobaki italipwa baada ya kipindi cha Mtazamio ya Marekebisho. |



J.K

Kiasi cha fedha anachodai Mkandarasi chini ya cheti cha muda kitalipwa na Mwajiri kwa Mkandarasi katika kipindi cha **siku 28** baada ya idhini ya cheti cha malipo wakati wa Mkataba kutolewa na Mhandisi.

25.3 **Malipo ya Mwisho**

Cheti cha malipo ya mwisho kitatolewa ndani ya siku **28** za kazi baada ya nyaraka hiyo kuidhinishwa na Mwajiri, ilimradi kazi zote, marekebisho yote na matengenezo yote kama yapo yatakuwa yametekelezwa pamoja na Mhandisi kujiridhisha

25.4 **Ucheleweshwaji wa Malipo**

Kama mwajiri atashindwa kufanya malipo ndani ya hamsini na katika muda uliotajwa, Mwajiri atamlipa Mkandarasi riba katika kiwango kilichotajwa kwenye **MMM**.

25.5 **Makato ya Malipo**

Mwajiri atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi chochote, fedha ya awali au madeni yanayolipika kutoka kwa Mkandarasi kwenda kwa Mwajiri kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa Mkandarasi na Mwajiri chini ya mkataba huu au mkataba mwingine ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria au pengine Mwajiri anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

25.6 **Malipo kwa Wafanyakazi**

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha mitambo/zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mwajiri atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya Mkandarasi.

25.7 Mwajiri atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa Mkandarasi mishahara yao na fidia nyingine na ada za kukodisha maunzi. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na Mkandarasi kutoka kwa Mwajiri chini ya mkataba huu.



AA J.K

| | |
|---|---|
| **26.** | **Malipo ya Ucheleweshaji kazi** |
| | Kama Mkandarasi atashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wo wote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, Mkandarasi atamlipa Mwajiri malipo ya ucheleweshaji wa kazi katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku au kiwango cha juu cha asilimia 15 ya bei ya mkataba. |
| **27.** | **Usuluhishaji wa Migogoro** |
| | 27.1 Kama migogoro ikitokea ndani ya mkataba huu, upande wowote utatoa Notisi ya Usuluhishi wa Mgogoro kwa njia ya majadiliano. Pande zote za mkataba, ndani ya siku ishirini na nane (28) baada ya siku ya kutolewa kwa notisi, zitahakikisha zinasuluhuisha migogoro hiyo kwa njia majadiliano ya pamoja. Endapo, migogoro hiyo ikashindwa kusuluhishwa, upande wowote unaweza kuwasilisha mgogoro huo kwa msuluhishaji wa nje alipendekezwa na Mamlaka kama ilivyobainishwa katika **MMM**.<br><br>27.2 Msuluhishaji aliyetajwa katika **MMM** atatoa maamuzi kwa maandishi au kwa njia la kielektroniki ndani ya siku ishirini na nane (28) baada ya kupokea notisi ya mgogoro.<br><br>27.3 Endapo maamuzi ya msuluhishaji hayatoridhiwa na upande wowote wa mkataba, Upande huo ndani ya siku zilizoainishwa katika **MMM** utawasilisha mgogoro huo katika hatua za juu za usuluhishi (arbitration). Endapo upande huo hautowasilisha mgogoro huo katika hatua za juu za usuluhishi (arbitration) ndani ya muda uliobainishwa katika **MMM**, maamuzi ya msuluhishi wa awali yatakuwa ya mwisho na yatatakiwa kuzingatiwa na pande zote za mkataba.<br><br>27.4 Mgogoro au utofauti wowote uliotolewa na Notisi ya Usuluhishi kwa njia ya Msuluhishaji wa Juu (Arbitration) kulingana na MJM utasuluhishwa kwa njii hiyo. Usuluhishaji huo utatekelezwa baada ya kutolewa kwa huduma chini ya mkataba.<br><br>27.5 Usuluhishaji huu (Arbitration) utatekelezwa kulingana na taratibu za |



XA J-K

| | |
|---|---|
| | usuluhishi zilizotolewa na taasisi ilitajwa na mahali palipotajwa katika **MMM.**<br><br>27.6 Bila kujali rejea yoyote uamuzi wa migogoro iliyomo humu,<br>(a) Pande za mkataba zitaendelea kutekelezwa majukumu yake ya mkataba, isipokuwa kama wakikubaliana vinginevyo; na<br>(b) Mteja atalipa fedha yoyote anazodaiwa na MH.<br><br>27.7 Kiwango cha ada ya Msuluhishaji na gharama za usuluhishi zitabebwa na pande zote za mkataba kwa usawa. Viwango na gharama hizo zitabainishwa kulingana na kanuni zitakazotolewa na Mamlaka iliyoteuliwa. Baada ya kukamilika kwa usuluhishi, kila upande utahusika na gharama na matumizi yake.<br><br>27.8 Endapo ikatokea Msuluhishaji amejiuzuru au kufa, au Mteja na MH wamekubaliana kuwa Msuluhishaji ameshindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na vifungu vya mkataba, Msuluhishaji mpya atateuliwa na Mamlama teuzi. |
| **28.** | **Uvunjaji wa Mkataba** |
| | 28.1 Kama Mkandarasi atashindwa kuanza kazi katika muda uliopangwa au kuwepo kwa sababu za kuaminika kuwa hatokamilisha huduma katika muda uliopangwa, kuwepo kwa ucheleweshaji utakaokiuka tarehe ya kukamilisha kazi, kushindwa kufuata moja ya masharti ya mkataba, kutofuata maelekezo ya Mhandisi au kufilisika, Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri Mkandarasi mpya wa kutekelezwa kandarasi husika.<br><br>28.2 Kama Mwajiri atashindwa kumlipa Mkandarasi ndani ya muda wa siku sitini (60) baada ya tarehe ya kutolewa Cheti cha Mhandisi Mkandarasi anaweza kuvunja mkataba. |
| **29.** | **Malipo Endapo Mkataba Umevunjwa** |
| | Pale mkatba utakapovunjwa, Mkandarasi atalipwa na TN kiwango cha fedha au bidhaa ambazo hazijajumuishwa katika malipo ya mkandarasi, kwa |



AA J-K

| | |
|---|---|
| | kandarasi zilizotekelezwa kabla ya tarehe ya kuvunjwa kwa mkataba kwa kima na bei zilizobainishwa katika mkataba. |
| **30.** | **Utoaji Majukumu (Assignment)** |
| | Mkandarasi hatogawa majukumu au sehemu ya majukumu yake ya kimkataba, bila kuwepo kwa makubaliano ya kimaandishi ya mwajiri. |
| **31.** | **Notisi** |
| | 31.1 Notisi inayotolewa na upande mmoja wa mkataba kwenda kwa upande mwingine kulingana na mkataba huu,<br>31.2 Notisi itakuwa hai pale inapowasilishwa katika tarehe ya notisi hiyo. |
| **32.** | **Kubadilika kwa Sheria na Kanuni** |
| | Ikiwa baada ya tarehe ya mwaliko wa kotesheni, sheria yoyote au kanuni za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania zitabadilika (ambazo zitategemewa na mamlaka kuhusisha mabadiliko yoyote ya tafsiri au matumizi) na kuathiri muda na/au bei ya mkataba, hivyo mabadiliko hayo yatapelekea muda au bei ya mkataba huo kuongezeka au kupungua, kwa kuzingatia kuwa Mkandarasi ameathirika katika kutekelezwa majukumu yake ya kimkataba. |

**IV) FOMU YA KUWASILISHA ZABUNI;**

**FOMU YA ZABUNI**

Kwa: KATIBU WA BODI YA ZABUNI
OFISI YA WAZIRI MKUU (SBUKVAU)
S.L.P. 980 DODOMA

Naahidi/Tunaahidi kutekeleza kazi ya Ujenzi/Ukarabati wa Majengo ya Vyuo Ufundi na Marekebisho ya Watu Wenye Ulemavu. Zabuni Na. **ZABUNI NA ME. 003/2021-22 /W/8** kulingana na Masharti ya Mkataba yanayofuatana na zabuni hii kwa bei ya Mkataba ya shilingi Milioni Mia Hamsini na Tisa, Mia Mbili Ishirini na Saba elfu, mia Tatu Arobaini (kwa maneno), (kwa tarakimu) 159,227,340.00 shilingi za kitanzania.

Pia tunaahidi kukamilisha kazi iliyotajwa katika kipindi cha [Ingiza kipindi] ~~siku~~/~~wiki~~/miezi Sita (Futa visivyo hitajika) ambacho kinajumuisha kipindi cha maandalizi.

Zabuni hii pamoja na barua yako ya kukubali kwa maandishi vitafanya mkataba unaotufunga sisi pamoja. Tunafahamu kuwa hulazimiki kukubali kiwango cha chini au zabuni yoyote kati ya zabuni unazopokea.

Tunathibitisha kuwa zabuni hii imetimiza masharti kama yanavyotajwa katika Mwaliko wa zabuni.

Saini Idhinishwa: [signature]

Jina la Mweka Saini: Anderson Allan

KD J-K

## V) BARUA YA WITO WA KUKUBALIWA ZABUNI.

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# PRIME MINISTER'S OFFICE
# POLICY, COORDINATION, PARLIAMENTARY AFFAIRS, LABOUR, EMPLOYMENT, YOUTH AND PERSONS WITH DISABILITY

**Telegraphic:** "WAZIRIMKUU"
**Tel No:**+255 (026) 2324534/- 026 293450/51
Fax No: +255 (262) 2324534
**Email:**ps@pmo.go.tz

Government City Mtumba,
P. O. Box 980,
**DODOMA.**

***In reply please quote:***

**Ref. No.** NA 365/294/01/83

04th January,2022

The Principal,
Dar es Salaam Institute of
Technology (DIT),
P. O. Box 2958,
**DAR ES SALAAM.**

Re**: LETTER OF ACCEPTANCE FOR TENDER NO. ME 003/2021-22/W/8-12 FOR RENOVATION AND EXTENSION WORKS FOR PRIME MINISTER'S OFFICE PERSONS WITH DISABILITY TRAINING CENTRES**

Refer the heading above.

2. This is to notify you that your bid for execution of the Tender No. ME 003/2021-22/W/8-12 for Renovation and extension works for Prime Minister's Persons with Disability Training Centre in respect to the above mentioned contract have been accepted by us. After successful negotiation we have agreed that the total contract price is **Tanzania Shilling Seven Hundred Sixty Nine Million, Seven Hundred Sixty Nine Thousand, Sixty Eight and fifty cents only (TZS. 765,769,068.50) VAT Exclusive.**

3. The Breakdown of total Contract Price as per individual Tender is as follows:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | ME 003/2021-22/W/08 | - Yombo | Tzs. 142, 450, 784 |
| ii) | ME 003/2021-22/W/09 | - Masiwani | Tzs. 97,988,240 |
| iii) | ME 003/2021-22/W/10 | - Luanzari | Tzs. 146,936,429.50 |
| iv) | ME 003/2021-22/W/11 | - Mtapika | Tzs. 141,441,216 |
| v) | ME 003/2021-22/W/12 | - Sabasaba | Tzs. 240,952,399 |

4. We confirm that Tanzania Institute of Arbitration be appointed as the Adjudicator.

5. You are here by instructed to confirm in writing before proceeding with execution of the said contract.

6. Thank you for your interest in this tender and we look forward to work with you on this contract.

Authorised Signature: ______________________

Name and Title of signatory: **Prof. Jamal A. Katundu – Acting Permanent Secretary**

Name of the Agency: **Prime Minister's Office, Policy, Coordination, Parliamentary Affairs, Labour, Youth, Employment and Persons with Disability**

**CC:** Chief Executive Officer,
Public Procurement Regulatory Authority,
P. O. Box 2865,
**DODOMA.**

Controller and Auditor General,
National Audit Office,
P. O. Box 9080,
**DAR ES SALAAM.**

Attorney General,
Attorney General Chamber,
Ministry of Justice and Constitutional Affairs
P. O. Box 630,
**DODOMA.**

Internal Auditor General,
Ministry of Finance and Planning,
P. O. Box 2802,
**DODOMA.**

J. K

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF**
**EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

# DIT INSTITUTE CONSULTANCY BUREAU (DIT ICB)

*When responding please refer*
Ref No: DIT-ICB/PMO/2022/01/01

**5th January, 2022**

**Permanent Secretary**
Prime Minister's Office
(Policy, Coordination, Parliament, Labour, Youth, Employment and People with Disabilities),
2 Railway Street,
P. O Box 980,
**40480 Dodoma**

Dear Sir,

RE: LETTER OF ACCEPTANCE FOR TENDER NO. ME.003/2021-22/W/8-12 FOR RENOVATION AND EXTENSION WORKS FOR PRIME MINISTER'S OFFICE PERSONS WITH DISABILITY TRAINING CENTRES.

SUB: LETTER OF ACCEPTANCE

Reference is made to the above heading and your letter with reference No. NA. 365/294/01/83 date 4th January 2022 concerning award of the above project.

This is to inform your good office that, we have received the above refered letter and we here by accept the award of the above project at a contract price of TZS 769,769,068.50 (Tanzanian Shilling Seven Hundred Sixty Nine Million, Seven Hundred Sixty Nine Thousand, Sixty Eight and Fifty Cent only. This amount is VAT Exclusive. Duration of the project is Six (6) Months.

Thanking you in advance, and we are looking forward to have a fruitfully business association with your good office for this assignment and for others in near future,

Yours Sincerely

Eng. Dr. Johnson L. Malisa
DIT Institute Consultancy Bureau Manager
**Dar Es Salaam Institute of Technology (DIT)**

**VI) UAINISHAJI VIWANGO NA VIPIMO KIUFUNDI, KAMA UPO;**

## VII) MAELEZO YA MAHITAJI NA ORODHA YA GHARAMA;

## SCHEDULE OF LABOUR

**GHARAMA ZA UFUNDI UJENZI WA CHUO CHA WATU WENYE ULEMAVU YOMBO ~~KASULU KIGOMA~~ DAR ES SALAAM**

| Na. | AINA YA KAZI | KIASI / UKUBWA | UNIT | BEI YA UFUNDI (LABOUR CHARGE) - TZS |
|---|---|---|---|---|
| A | **Msingi wa Jengo (Sub-structure)** | | | 39,806,835.00 |
| | Kusafisha eneo | | | |
| | Kuseti jengo | | | |
| | Uchimbaji wa msingi pamoja na "Columns base" | | | |
| | Kufukia | | | |
| | **Usukaji wa Nondo katika;** | | | |
| | 'Base Columns" | | | |
| | Nguzo za Msingi | | | |
| | 'Ground beams" | | | |
| | **Kufunga mbao** | | | |
| | Pembezoni mwa jamvi | | | |
| | Pembezoni mwa nguzo pamoja na pembeni mwa base Columns | | | |
| | Kuondoa mbao | | | |
| | **Kumwaga zege** | | | |
| | Chini kwenye msingi | | | |

ENGINEERS REGISTRATION BOARD
TANZANIA
INSTITUTE CONSULTANCY BUREAU (DIT)
P.O.Box 2958 - DAR-ES-SALAAM
Engineering Consulting Firm No. 057 L
SIGN .................... DATE ....................

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Chini kwenye msingi wa nguzo | | | |
| | Katika nguzo ya awali | | | |
| | Kwenye jamvi pamoja na "beams" | | | |
| | Ujenzi wa tofali za msingi | | | |
| | **Mawe** | | | |
| | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | | | |
| | Umwagiliaji wa maji | | | |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | | | |
| **B.** | **Kunyanyua jengo (Super-structure)** | | | 71,612,303.00 |
| | Ujenzi wa tofali za kuta na uwekaji DPC | | | |
| | **Kufunga mbao katika:** | | | |
| | Nguzo mlalo | | | |
| | Nguzo wima | | | |
| | 'Suspended Slab" ,Gutter ya Zege, Ngazi Pamoja na Ramp | | | |
| | **Kusuka nondo katika:** | | | |
| | Nguzo mlalo | | | |
| | Nguzo wima | | | |
| | 'Suspended Slabs" | | | |
| | Ngazi, Ramp pamoja na Gutter | | | |
| | **Kumwaga zege katika:** | | | |
| | Nguzo mlalo | | | |
| | Nguzo wima | | | |
| | 'Suspended Slab", "Ramp", Gutter pamoja na Ngazi | | | |

XA J-K

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Umwagiliaji wa maji | | | |
| | **Jumla ndogo Kunyanyua jengo (Super-structure)** | | | |
| | | | | |
| **C.** | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | | | 31,845,468.00 |
| | Kuezeka | | | |
| | **Jumla ndogo Kuezeka** | | | |
| | **Jumla ndogo Rangi na mapambo** | | | |
| **H.** | **Umeme (Electrical installation)** | | | 6,369,094.00 |
| | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | | | |
| | **Jumla ndogo Umeme** | | | |
| | | | | |
| **J.** | **Tehama** | | | 1,592,273.00 |
| | Usukaji wa mifumo ya tehama awamu ya kwanza - Conduit na Box | | | |
| | **Jumla ndogo Tehama** | | | |
| **K.** | **Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)** | | | 7,961,367.00 |
| | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | | | |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na taka** | | | |
| | | | | |
| | **GHARAMA ZA UFUNDI UJENZI WA CHUO CHA WATU WENYE** | | | |

ENGINEERS REGISTRATION BOARD
TANZANIA
INSTITUTE CONSULTANCY BUREAU (DIT)
P.O.Box 2958 - DAR-ES-SALAAM
Engineering Consulting Firm No. 057 L
SIGN............ DATE............

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **ULEMAVU KASULU KIGOMA** | | | |
| | **MAJUMUISHO (SUMMARY)** | | | **TZS** |
| | | | | |
| **A.** | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | | | 39,806,835.00 |
| **B.** | Kunyanyua jengo (Super-structure) | | | 71,845,468.00 |
| **C.** | Kuezeka (Roof structure and covering) | | | 31,845,468.00 |
| **H.** | Umeme (Electrical installation) | | | 6,369,094.00 |
| **J.** | Tehama | | | 1,592,273.00 |
| **K.** | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | | | 7,961,367.00 |
| | **JUMLA KUU** | | | 159,227,340.00 |

ENGINEERS REGISTRATION BOARD
TANZANIA
INSTITUTE CONSULTANCY BUREAU (DIT)
P.O.Box 2958 - DAR-ES-SALAAM
Engineering Consulting Firm No. 057 L
SIGN ............ DATE ............

AA

J.K

## IX) MHUTASARI WA MAJADILIANO.



KA

J-1K

# RECORD OF NEGOTIATIONS

**Name of the Procuring Entity:** Prime Minister's Office

**Bid ID No.:** ME/003/2021-2022/W/5, ME/003/2021-2022/W/6, ME/003/2021-2022/W/7, ME/003/2021-2022/W/8, ME/003/2021-2022/W/9, ME/003/2021-2022/W/10, ME/003/2021-2022/W/11, ME/003/2021-2022/W/12.

**Subject of Procurement:** Proposed Renovation, Extension and New Construction of Personal with Disability Training Centres for Prime Minister's Office at Kasulu-Kigoma, Kisesa- Mwanza, Mbozi-Songwe, **Yombo-Dar es salaam, Masiwani –Tanga, Luanzari-Tabora, Mtapika-Masasi and Sabasaba-Singida**. (Vote 37).

**Method of Procurement:** Single Source

**Date of Negotiation:** Wednesday 28th December, 2021 at 12:00 hour's local time

| PART 1: RECORD OF NEGOTIATIONS | |
|---|---|
| **ISSUE** | **AGREEMENT (WITH FULL DETAILS)** |
| Bidding Price | The Contractor has agreed to reduce the contract prices as follows: -<br>Yombo-Dar es salaam from 152,625,840.00 to 142,450,784<br><br>Masiwani –Tanga From 104,987,400.00 to 97,988,240.00<br><br>Luanzari-Tabora from 157,431,888.75 to 146,936,429.50<br><br>Mtapika-Masasi from 151,544,160.00 to 141,441,216.00<br><br>Sabasaba-Singida. From 258,163,284.03 to 240,952,399.00 |
| Programme of work | The Contractor has submitted programme of work as per bidding document |
| Quoted Price in Each Item | The Contractor has failed to quote in each item because the quantities ware not |

| | |
|---|---|
| | provided in schedule of labour |
| Detailed of submitted Scheduled of Labour | The Contractor has not submitted the detailed schedule of labours because no quantities were provided |
| Work Schedule to accommodate any changes | The Contractor has confirmed to accommodate any changes pre to agreement between the two parties |
| Confirmation on Contract Sum. | The Contractor agreed on Contract Sum as follows: -<br>Yombo-Dar es salaam 142,450,784.00<br>Masiwani –Tanga 97,988,240.00<br>Luanzari-Tabora 146,936,429.50<br>Mtapika-Masasi 141,441,216.00<br>Sabasaba-Singida 240,952,399.00<br>**Total 769,769,068.50**<br>(Tanzanian shillings Seven Hundred Sixty-Nine Million, Seven Hundred Sixty-Nine Thousand, Sixty-Eight and Fifty Cents Only) VAT Exclusive with completion period of Six (6) months and Defect liability Period of Six (6) Months. |

We hereby certify that the above is a true and accurate record of the negotiations:

| For the Procuring Entity | For the Bidder |
|---|---|
| Signature: [signature] | Signature: [signature] |
| Name: WENCESLAUS LAMBILEKI | Name: Anderson Allan Tovir |
| Position: MWENYEKITI | Position: Architect |
| Date: 28/12/2021 | Date: 28-12-2021 |

**Document attached:**
Minutes of the Negotiation meeting



AA JK